**Noa Bongo!Jenga Maisha Yako!**

**Utandawazi : Uhamiaji na Tatizo la Kujumika kwenye Jamii Ujerumani**

**Autorin :(O-Ton +Text): Sandrine Blanchard**
**Redaktion :Yann Durand**
**Übersetzung : Anne Thomas**

---

**3 Stimmen – Sauti 3 :**

**-junger Sprescher 1 …………….Msimulizi wa kiume 1**
**-junge Sprecherin 1 ……………. Msimulizi wa kike 1**
**-Sprescher(in) 2 ………………….Msimulizi wa kike 2**
**als Off Stimme für die Reportage**

**Für die O-Töne dazu :**
**5 Männer : Wanaume 5**
**1 Frau : Mwanamke 1**

---

**Vorspann LbE………………………..Kiashirio cha Kipindi**

**SEHEMU YA KWANZA - REPORTAGE : REPOTI**

**Msimulizi wa kike 1 :** Habari gani! Natumai nyote hamjambo !

**Msimulizi wa kiume 1:** Leo katika mfululizo wetu wa Noa Bongo!Jenga Maisha Yako! juu ya utandawazi tutazunngumzia juu ya matatizo wanayoyakuta Waafrika wanaoishi nchini Ujerumani katika maisha yao.

**Msimulizi wa kike 1 :** …………matatizo yao ni kujiambatanisha na kujumuika katika jamii…..

**1.Atmo Afroshop unterlegen …………duka la Kiafrika……..**

**Msimulizi wa kiume 1 :** Tunaelekea Ujerumani na hasa katika mji wa Bonn ambapo tutalitembelea duka moja la Kiafrika…….

**Msimulizi wa kike 1 :** ……duka ambalo unaweza ukapata bidhaa kutoka Afrika pamoja na kukutana na Waafrika ……

**Msimulizi wa kiume 1 + Msimulizi wa Kike 1 :**

Kwa hiyo fungeni mikanda yenu tayari kwa safari!

**………………..Manuskript…………………….**

**Msimulizi wa kike 1 :** 'Treichville,Soko la Kimataifa,bidhaa za kigeni na vipodozi' hivyo ndivyo lilnavyosema bango lilioko nyuma ya jengo moja kubwa ambako ndiko ilioko ofisi ya huduma za utawala mjini Bonn.Kwa maneno mengine tunaweza kusema kisiwa kidogo cha Afrika kiko nyuma ya ukumbi wa jiji.

**1.Atmo hoch ………………….**

**2.O-Ton Juste**

Nimezaliwa nchini Cameroon na daima nitakuwa Mcameroon.

**Msimulizi wa kike 2:** Juste amefunga ndoa na mwanamke wa Kijerumani na kuchukuwa uraia alionao mke wake ili kurahisisha taratibu za kiutawala.Imebidi aikane paspoti yake ya Cameroon.

**Msimulizi wa kike 2:** Ndani ya duka hilo la Afroshop masuala juu ya maisha nchini Ujerumani yanachochea mjadala mkali.Ciceli ni mhandisi ambaye ameishi zaidi ya miaka 20 nchini Ujerumani.Anasema ni nadra kwa wahamiaji kuhjijichagulia hasa mahala pao pa kuishi uhamishoni.

**4.O-Ton Cecile Qualifizierte : 0:38**

Iwapo sisi Waafrika,wageni tunakuja hapa na tunakuwa na ujuzi mkubwa wa kitaalamu ni kwa ajili ya kuendeleza maarifa yetu na badaae kurudi nyumbani.Hapa ni pabaya zaidi kuliko hata

nyumbani.Waafrika wanakuja hapa na stashahada zao ni wanataaluma hasa na hufanyishwa kazi za kusafisha.Hivyo wazazi wako wamekupeleka shule ili uje kukosha vyoo? Kweli hilo ni jambo la kawaida?Tumekuwa ombaomba wa daima siku sote tukisema samahani kwa kuuliza ……inachosha sana.

**Msimulizi wa kike 2 :** ……..Cecile amewapiga marufuku watoto wake kuja kusoma Ulaya.Badala yake yuko tayari kuwatumia pesa ili kwamba waendelee kusoma barani Afrika.Lakini Yannick ambaye ni mwanafunzi hakubaliani na mashaka yake hayo.

**4.O-Ton Yannick Jugendlische :**

Kizazi ambacho ninakifamu kiko wazi kabisa.Ni kizazi kipya. Kile ambacho Waafrika wengine wamekuwa wakinieleza ni vigumu sana kuelewa………..

**Msimulizi wa kike 2 :** David ni mwananchi wa Ivory Coast anasema sitafahamu inatokea kati ya Wazungu na Waafrika kwa sababu hawafahamiani vya kutosha……

**5.O-Ton David Reichtum : 0.24 …………………………….**

Kwa mfano leo hii walikuwa wakilalamika kwamba vijana wa Kiafrika wanakuja kufa kwenye fukwe za Lampedusa.Lakini katu hatukuwahi kuonyesha sura mbaya ya Ulaya huko Afrika. Siku zote tumekuwa tukionyeshwa kwamba Wazungu wote wanaishi kama wana wa wafalme katika utajiri uliozagaa. Kwamba hakuna watu maskini hapa.Hicho ndicho tunachoambiwa barani Afrika kuhusu Ulaya .

**Msimulizi wa kiume 1 :** Kwa nini Waafrika wanaoishi Ujerumani hawaelezi ukweli juu ya maisha yao vijana ambao bado wako nyumbani?

**6.O-Ton David Absurd ……………..**

Ni kweli ! Huwa ninawakusanya vijana huko Afrika na kuweleza juu ya Ujerumani,kuhusu Ulaya na jinsi mambo yalivyokuwa magumu hapa…….Nawaambia wasikubali kufa baharini wakati wakiwa safarini kuja huku …..lakini wakati wa jioni kwenye televisheni wanawaona vijana wa Kijerumani au vijana wa Kifaransa wakiwa kwenye fukwe au wakiendesha magari ya kisasa kabisa na kadhalika ……….kidogo inakuwa kama ni upuuzi.

**Msimulizi wa kiume 1 :** Vipi kuhusu wale wahamiaji wanaojificha ?

**Msimulizi wa kike 1 :** Tulijaribu kuzungumza na watu watatu ambao hawana makaratasi ya kisheria lakini waligoma kurekodiwa sauti zao. Walikuwa wanaogopa wasije kutambuliwa.Maisha yao ni moto, siku zote wanakuwa wanajificha ficha kwa kuhofia kukamatwa.

**Msimulizi wa kike 2 :** Mmmojawapo wa watu hao wanaotembelea mara kwa mara duka la Afroshop mjini Bonn ambaye pia alikuwa hataki kutajwa jina lake anaelezea jinsi inavyokuwa rahisi kwa mtu kuishia kuwa mhamiaji wa kuzamia na kujificha dhidi ya mkono wa sheria.

**7.O-Ton Illegale 0:32 ( mhamiaji sio halali)**

Baada ya mwaka mmoja kunakuwa hakuna tena pesa zaidi kwani inabidi ulipe kodi ya nyumba,bima na kadhalika.Iwapo huna cheti cha lugha inabidi uende mahala kwengine ambapo hauna haja ya kumuangalia mtu usoni.Unafikia mahala ambapo unakuwa huna tena la kufanya kwamba inabidi uwe mhamiaji usie halali.Unaishia kulala kwenye vituo,huna nyumba,huna chochote kile.Na unaanza kujiuliza mwenyewe nimefanya nini kustahiki yote haya?Hivyo mimi sio binaadamu ?

**Msimulizi wa kiume 1 :**
Kwa hiyo wahamiaji wasiokuwa na makaratasi wanaoishi kinyume na sheria wanaendelea kubakia Ulaya kwa sababu wanaona aibu kurudi nyumbani na kukiri kwamba wameshindwa.
**Msimulizi wa kike 1 :** Ndio hiyo mara nyingi inakuwa mojawapo ya sababu.

**Msimulizi wa kiume 1 :** Lakini kumekuwepo na Waafrika walioko kwa muda mrefu barani Ulaya.Lazima watakuwa wamepoteza uwelewa wa hali halisi ilioko katika nchi walikozaliwa au vipi ?

**Msimulizi wa kike 2 :** Karibu wale wanaolitembela sana duka la Kiafrika la Afroshop bado wangali wana ndoto ya kurudi nyumbani.Lakini mmoja kati yao anasema kwamba wamedanganyika na wamekuwa tu wakikataa kungalia ukweli.

**8.O-Ton Bleiben 0.31 …………Mhamiaji aliebakia**

Mimechoka kuzisikia hadithi hizi.Mimi ni Muafrika na sitaki kurudi Afrika. Kwa nini ?Kwa sababu kwa sasa nawafanyia kazi Wajerumani.Kuna Waafrika wengine hapa ambao wanasema uongo.Wale wanaosema wataondoka hapo kesho wanyoshe mikono yao…….

**Wateja wengine dukani :**

Mimi naondoka… ..naondoka!….natoka Cameroon lakini nimekuwepo hapa kwa muda mrefu.Ujana wangu wote umepotea hapa.Nina kitu gani Cameroon?Siijuwi Cameroon.Kitu pekee ninachokijuwa juu ya Cameroon ni kwamba ninakwenda huko kwa mapumziko ya wiki tatu kwa mwaka.Hakuna zaidi ninachokijuwa.Marafiki zangu wako hapa,familia yangu iko hapa.Huwezi kusema ninapaswa kurudi Cameroon.

**MWISHO WA SEHEMU YA KWANZA**

**Musik hoch dann unterlegen und ausbelenden………………….**

**SEHEMU YA PILI ERKLÄRSTÜCK …………**

**Msimulizi wa kiume 1 + Msimulizi wa kike 1 tu …..**

**Msimulizi wa kiume :** Je ni kweli wahamiaji wasio halali huwa wanafunga ndoa na watu wasiowajuwa ili tu kwamba waweze kubakia Ulaya ?

**Msimulizi wa kike :** Hiyo ndio ile ndoa inayojulikana kuwa ya bandia au ya ulaghai. Nchini Ujerumani na katika nchi nyengine za Umoja wa Ulaya ndoa hizi sio halali lakini ni utaratibu ulio bado mashuhuri.

**Msimulizi wa kiume :** Lakini pia kuna ndoa zinazotokana na mapenzi kati ya Waafrika na Wazungu,

**Msimulizi wa kike :** Bila ya shaka.Unaweza kupata ukaazi wa kudumu baada ya kuishi na mtu fulani kwa miaka miwili na pia unaweza kuomba uraia wa Ujerumani baada ya miaka miwili au mitatu.

**Msimulizi wa kiume :** Vipi kuhusu wale ambao hawakufunga ndoa na raia wa Kijerumani ?

**Msimulizi wa kike :** Kuna hatua mbali mbali za kuchaguwa kufuata : iwapo mhamiaji ana familia na amekuwa akiishi nchini Ujerumani kwa miaka sita ………anaweza kuomba uraia.

**Msimulizi wa kiume :** Inakuwaje iwapo familia imebakia Afrika?

**Msimulizi wa kike :** Katika kesi kama hiyo inabidi awe amebakia Ujerumani angalau kwa miaka minane mfululizo.Venginevyo awe ameshiriki madarasa ya kujumuishwa kwenye jamii na hapo anaweza kuomba uraia wa Kijerumani baada ya miaka saba.Madarasa hayo ya kujumuishwa kwenye jamii yanafundisha lugha ya Kijerumani,historia na utamaduni.

**Msimulizi wa kiume :**Hayo ni masharti !

**Msimulizi wa kike :** Kwa muda mrefu ilikuwa ni lazima uwe na angalau mzazi mmoja wa Kijerumani ili kuweza kupata uraia wa Ujerumani.Hiyo ilikuwa ikijulikana kama haki ya damu.

**Msimulizi wa kiume :** Nina suali jengine.Unaweza kushikilia uraia wako wa asili iwapo unakuwa raia wa Ujerumani?

**Msimulizi wa kike :** Kwa jumla hapana.Lakini Ujerumani imefikia makubaliano na nchi fulani.Hata hivyo kwa kawaida unapokuwa Mjerumani inabidi uachane na uraia wako wa asili.

**Msimulizi wa kiume :** Vipi kuhusu wakimbizi ? Wale ambao wanakandamizwa katika  nchi zao?

**Msimulizi wa kike :** Serikali ya Ujerumani huchunguza kesi zao.W akati huo huo kuwepo kwao nchini kunavumiliwa.Baadae aidha hadhi yao ya ukimbizi inatambulika na baadae kujumuishwa kwenye jamii au maombi yao ya kupatiwa hifadhi hukataliwa na hapo tena husindikizwa kurudishwa makwao.

**Msimulizi wa kiume :** Kwa hiyo njia bora kabisa ya kuingia Ulaya ni kuwa mtu mwenye ujuzi wa kitaaluma ?

**Msimulizi wa kike :** Ndio ni sawa kabisa. Umoja wa Ulaya unatafuta wafanyakazi wenye ujuzi katika sekta fulani.Kwa hiyo baadhi ya watu inakuwa rahisi kupenya kwenye soko la ajira na yumkini wakaweza kubakia moja kwa moja.

**Outro ……………………..Funga kipindi……..**

Na kufikia hapo ndio tumefika mwisho wa kipindi chetu cha Noa Bongo!Jenga Maisha Yako!Ahsante kwa kusikilizakipindi hiki juu ya utandawazi na tatizo la kujumuika kwenye jamii nchini Ujerumani .Ni kipindi cha Deutsche Welle kilichotayarishwa na Sandrine Blanchard. Ili kujuwa zaidi au iwapo unataka kusikiliza tena kipindi hiki tafadhali nenda kwenye tovuti yetu : www.dw-world.de/lbeUsikose kujiunga nasi tena mara nyengine!
Kwaheri !